**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UVUVI 2020



*“Natoa wito kwa wavuvi na wananchi wote kwa ujumla kuzingatia marekebisho ya Kanuni hizi”*-
**Dkt. Rashid Tamatamah, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)**



## 1. Marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2019 – GN 383

| MAREKEBISHO | SABABU ZA KUFANYA MAREKEBISHO |
|---|---|
| Serikali imeruhusu matumizi ya leseni moja ya uvuvi katika kila eneo la maji badala ya leseni kutolewa na kila Halmashauri. | Kupunguza gharama za uendeshaji kwa wavuvi ambapo walikuwa wanalazimika kukata leseni zaidi ya moja kila wanapofanya shughuli za uvuvi katika Wilaya au Halmashauri nyingine. |
| Serikali imeruhusu matumizi ya nyavu za dagaa zenye ukubwa wa macho ya milimita 8 badala ya 10 kwenye maji chumvi. | Utafiti ulionesha kwamba nyavu za mm 10 kwa uvuvi wa dagaa katika maji chumvi hauna tija kwa mvuvi kwani mapato yalikuwa hayakidhi gharama za uendeshaji. |
| Serikali imeondoa ukomo wa samaki aina ya Sangara wazazi (zaidi ya cm 85) wanaotakiwa kuvuliwa kutokana na kuongezeka kwa samaki. | Tafiti zilibainisha ongezeko kubwa la samaki wazazi aina ya Sangara (zaidi ya cm 85) kufuatia kuimarika kwa ulinzi wa raslimali za uvuvi nchini. |
| Serikali imeruhusu kuvuliwa kwa Kaa wenye uzito wa gramu 450 badala ya gramu 500 kama ilivyokuwa awali. | Tafiti zilibainisha kuwa Kaa mwenye uzito kuanzia gramu 450 amefikia kiwango cha kuvunwa na kuuzwa kibiashara. |

## 2. Marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2020 – GN 492

| MAREKEBISHO | SABABU ZA KUFANYA MAREKEBISHO |
|---|---|
| Serikali imeruhusu matumizi ya taa za nishati ya jua (Solar) katika shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa wavuvi. | Tafiti zimebainisha kwamba matumizi ya taa za solar zenye jumla ya watts 90 kwa chombo katika Ziwa Victoria na watts 50 kwa chombo katika Ziwa Tanganyika hazina madhara katika mazingira na ikolojia. |

| | |
|---|---|
| Serikali imeruhusu matumizi ya nyavu za makila zilizounganishwa (vertical integration) zenye macho yasiyozidi 78 kwa uvuvi wa Sangara Ziwa Victoria na macho yasiyozidi 144 kwa uvuvi wa Migebuka katika Ziwa Tanganyika. | Tafiti zimebaini kuwa matumizi ya nyavu hizo kwenye maji ya kina kirefu hayana madhara makubwa; na pia uvuvi huo unaongeza tija kwa wavuvi.<br><br>Kabla ya marekebisho hayo, nyavu zilizokuwa zinaruhusiwa kwa uvuvi wa Sangara ni zile za single zenye macho yasiyozidi 26.<br><br>Kwa upande wa Ziwa Tanganyika hakukuwa na kiwango cha idadi ya macho kwa nyavu za makila kwa uvuvi wa Migebuka. |
| Serikali imeruhusu matumizi ya nyavu za ringnet (mtando) katika Ziwa Tanganyika kwenye maji ya kina kirefu umbali wa mita 1,000 kutoka ufukweni, kisiwa au Peninsula kwa kutumia mwanga nyakati za usiku. | Tafiti zimebaini kuwa matumizi ya nyavu za ringnet kwenye maji ya kina kirefu na kwa kutumia nishati ya mwanga nyakati za usiku hazina madhara katika uendelevu wa rasilimali za uvuvi na ikolojia. |
| Serikali imeruhusu kuuza pweza waliochakatwa ambao wana uzito usiopungua gram 440. | Tafiti zimebaini kwamba Pweza aliyechakatwa kwa kuondolewa matumbo uzito hupungua kwa takribani gramu 60. Hivyo kwa kuwa sheria hairuhusu uvuvi wa Pweza chini ya gram 500, basi Pweza aliyechakatwa wa gramu 440 atakuwa amekidhi wiwango vya kuvuliwa akiwa amekomaa. |
| Serikali imeruhusu matumizi ya madema yenye macho yasiyopungua inchi 3'' katika shughuli za uvuvi kwenye maji ya asili. | Kanuni hii imewekwa ili kuwa na uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi nchini kwani matumizi ya madema chini ya nchi 3" kunasababisha kuvuliwa kwa samaki wachanga.<br><br>Kabla ya marekebisho haya hakukuwa na Kanuni ya kuonesha ukubwa wa macho ya madema yanayofaa katika shughuli za uvuvi. |

| | |
|---|---|
| Serikali kutoruhusu matumizi ya mitalimbo au michinji kwa uvuvi wa Pweza katika maji chumvi kwa kuwa zana hizo zinapunguza ubora wa Pweza na pia husababisha uharibifu wa mazingira na ikolojia ya bahari. | Kanuni hii imewekwa ili kuzingatia ubora wa zao la Pweza na kulinda mazingira. Zana inayotakiwa kutumika katika uvuvi wa Pweza ni mchokoo wa mti (wooden stick) na matumizi ya vyungu (pots) katika maeneo ya miamba ambapo Pweza hujiwekea makazi.<br><br>Kabla ya marekebisho haya hapakuwa na Kanuni ya kukataza matumizi ya mitalimbo au michinji kwa uvuvi wa Pweza katika maji chumvi. |
| Serikali kutoruhusu matumizi ya nyavu za ringnet (mtando) nyakati za mchana katika maji chumvi. | Mtego wa ringnet unatumika nyavu za macho madogo (Mf. Milimita 8) kuvua samaki jamii ya dagaa wanaopatikana katika tabaka la juu la maji kwa kutumia nishati ya mwanga nyakati za usiku. Hivyo matumizi ya nyavu hizo nyakati za mchana yatapelekea kuvuliwa kwa samaki wachanga wasiokusudiwa tofauti na dagaa. |
| Serikali kutoruhusu matumizi ya nyavu za mtando/ringnet kwenye eneo la kina cha maji kisichopungua mitaa 50 katika maji chumvi. | Utafiti umeonesha kwamba nyavu hizi zikitumika kwenye maeneo ya kina kifupi ambako ndio mazalio na makulio ya samaki zinasababisha uharibifu mkubwa ikiwemo kupungua kwa samaki kutokana na kukamata samaki wachanga wasiokusudiwa, na uharibifu wa ikolojia na mazingira kwa ujumla. |
| Serikali kutoruhusu matumizi ya nyavu halali ambazo zimechanganywa na nyavu haramu katika shughuli za uvuvi. | Kanuni hii imewekwa ili kuwa na uvuvi ambao ni endelevu.<br><br>Kabla ya marekebisho haya hapakuwa na Kanuni ya kudhibiti matumizi ya nyavu zilizochanganywa. |
| Serikali kuruhusu uvunaji wa Kambakochi jamii ya Scyllaridae (sandy lobster) kwa uzito usiopungua gramu 250. | Utafiti umeonesha kwamba jamii hii ya Kambakochi haikuwi zaidi ya gramu 350.<br><br>Kabla ya marekebisho haya hapakuwa na Kanuni inayoruhusu uvunaji wa Kambakochi jamii ya Scyllaridae (sandy lobster). |

| | |
|---|---|
| Serikali kutoruhusu matumizi ya generator katika shughuli za uvuvi. | Kiwango cha mwanga kinachozalishwa na generator kinaweza kuathiri ukuaji wa samaki na viumbe wengine wa majini (associated aquatic organisms).<br><br>Hata hivyo eneo hili limependekezwa kufanyiwa utafiti zaidi kuhusu madhara yanayotokana na matumizi ya generator katika shughuli za uvuvi na Wizara imeruhusu matumizi ya generator katika uvuvi mpaka tarhe 1 Januari 2021 yakisubiriwa majibu ya utafiti.<br><br>Kabla ya marekebisho haya hapakuwa na Kanuni inayoelekeza matumizi ya nishani itokanayo na generator katika shughuli za uvuvi. |

Imetolewa na

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**www.mifugouvuvi.go.tz**
**Simu: 0763 255255**